



East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 5, Issue 1, 2022

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Kimatumizi kwenye Kaunti ya Bungoma

Martin Barasa Mulwale^{1*}, Prof. Florence Ngesa Indede, PhD¹ na Dkt. Beverlyne Asiko Ambuyo, PhD¹

¹ Chuo Kikuu cha Maseno, S. L. P. 333, Maseno, Kenya.

*ORCID ID: <https://orcid.org/0000-0002-9871-4647>; Barua pepe ya mawasiliano: mulwalemartin@yahoo.com

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.665>

Tarehe ya Uchapishaji: **IKISIRI**

16 Mei 2022

Istilahi Muhimu:

*Uamilifu,
Sera ya Lugha,
Mawanda,
Ruwaza ya Lugha,
Ikolojia ya Lugha.*

Lugha ni chombo maalum katika ustawishaji na uimarishaji wa rasilimali za mwanadamu. Pia, ni wenzote unaohimili sera ambazo hulenga katika kutimiza matarajio ya kitaifa katika nchi yoyote ile. Nchini Kenya, vipengele katika katiba ya 2010, vinavyohusu lugha vilipandisha hadhi lugha ya Kiswahili ili iweze kutumika kama lugha ya taifa na rasmi sambamba na Kiingereza. Hata hivyo, katiba hii haijaweka kanuni zinazolenga kuimarisha na kudumisha uanuwai wa lugha za kiasili kote nchini Kenya. Machukulio ni kwamba, vipengele vya katiba vinasheheni sifa stahilifu kama vile, usawa wa kimatumizi, utekelezaji, mikao ya kieneo, matakwa, pamoja na hiari za wananchi. Kwa kuangazia hali ya kiisimu-jamii katika Kaunti ya Bungoma, utata upo katika udumishaji wa mfumo 'rasmi' wa sera ya lugha Kitaifa, na utekelezaji wa sera ya lugha kupitia asasi za serikali na zile za umma. Kazi hii inalenga kuchanganua uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu kupitia ruwaza zinazodhihirika katika mawanda mbalimbali ya lugha katika Kaunti ya Bungoma. Mihimili ya nadharia ya sera ya lugha iliyoendelezwa na Spolsky (2004, 2007) ambayo ni Usimamizi wa lugha na Ikolojia ya lugha pamoja na ruwaza za lugha ilivyoendelezwa na Paltridge (2001) ndiyo nguzo ya kuchanganua utafiti huu. Aidha, mtazamo wa Haugen (1972) unaohusu Ikolojia ya lugha umetumika katika kudhihirisha michakato baina ya lugha na mazingira inamotumika. Muundo mseto uliojumuishwa, muundo wa kimaielezo, kiupelelezi na wa kiiktisadi ulitumiwa. Usampulishaji dhamirifu ulitumiwa kuteua matumizi ya lugha ya KS, KB na KS/KB katika ruwaza za lugha zilizodhihirika katika mawanda ya biashara, kanisani na utawala hasa kwenye mikutano ya umma au baraza za Chifu katika maeneo mbalimbali ya Kaunti ya Bungoma. Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchunzaji usio-shirikishi na ya kiiktisadi ilikusanywa kwa kuhesabu hali ambazo lugha za KS,

KB au KS/KB zilitumiwa. Ilibainika kuwa lugha ya KS na KB hukamilishana kiuamilifu katika mawanda mbalimbali ya kijamii katika Kaunti ya Bungoma.

APA CITATION

Mulwale, M. B., Indede, F. N., & Ambuyo, B. A. (2022). Uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Kimatumizi kwenye Kaunti ya Bungoma. *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), 109-123. <https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.665>.

CHICAGO CITATION

Mulwale, Martin Barasa, Florence Ngesa Indede and Beverlyne Asiko Ambuyo. 2022. "Uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Kimatumizi kwenye Kaunti ya Bungoma". *East African Journal of Swahili Studies* 5 (1), 109-123. <https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.665>.

HARVARD CITATION

Mulwale, M. B., Indede, F. N., & Ambuyo, B. A. (2022) "Uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Kimatumizi kwenye Kaunti ya Bungoma", *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp. 109-123. doi: 10.37284/jammk.5.1.665.

IEEE CITATION

M. B. Mulwale, F. N. Indede, & B. A. Ambuyo. "Uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Kimatumizi kwenye Kaunti ya Bungoma", *EAJSS*, vol. 5, no. 1, pp. 109-123, May. 2022.

MLA CITATION

Mulwale, Martin Barasa, Florence Ngesa Indede & Beverlyne Asiko Ambuyo. "Uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Mawanda ya Kimatumizi kwenye Kaunti ya Bungoma". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 5, no. 1, May. 2022, pp. 109-123, doi:10.37284/jammk.5.1.665.

UTANGULIZI

Lugha ni chombo maalum katika ustawishaji na uimarishaji wa rasilimali za mwanadamu. Ni wenzu unaohimili ruwaza na sera ambazo hulenga katika kuafikia matarajio ya kitaifa katika nchi yoyote ile (Webb, 2002). Kwa mujibu wa Shitemi (2011), lugha hudumisha mahusiano ya kijamii, hutumika katika miktadha mbalimbali ya uamilifu katika mawanda mbalimbali ya kimawasiliano. Okombo (2001) anadai kuwa, jamii hutumia lugha ili kuimarisha ushirikiano miongoni mwa umma katika shughuli za maendeleo kupitia hatua mbalimbali za uhamasishaji. Hivyo basi, wanajamii wana uhuru wa kuteua lugha zilizo na umuhimu katika miktadha ya kitaifa, au zile ambazo wao wanaweza kuzitumia katika mawasiliano miongoni mwao kutegemea mahitaji yao ya kimsingi. Hii inatokana na hali kuwa, kuna majukumu ya lugha ya kijumla, na yale ambayo hujenga na kudumisha maelewano miongoni mwa watu, sambamba na kuweka viunzi vinavyodhihirisha uteuzi wa lugha kulingana na vipengele vya miktadha ya kimatumizi katika jamii (Lu, 1988). Katika hali hii, uamilifu wa lugha ni kiunzi kinachodhihirisha uhusiano wa kutegemeana, kutegemea muktadha baina ya hali mbili au zaidi zinazolingiana katika mazingira fulani.

Kimsingi, uamilifu wa lugha ni jumla ya nyenzo zinazoiwezesha lugha kuhimili na kutimiza majukumu mbalimbali kulingana na matarajio ya mtumiaji lugha katika jumla lugha husika. Kwa mujibu wa Romaine (2006), uamilifu ni kigezo cha kimsingi katika mifanyiko ya kimfumo inayojumuisha vipashio katika mfumo maalumu wa kiisimu kwa upande mmoja, na utendaji kazi wa lugha kwa upande mwingine. Hivyo basi, uamilifu wa lugha hutokea katika mfumo wa kijamii, na kila jamii hutegemea lugha kama wenzu wa mtagusano unaowezesha lugha kutumika katika kutimiza mahitaji mbalimbali ya kimawasiliano kwa njia adilifu na ya haki. Kutokana na maoni haya kazi hii inachunguza uamilifu wa Kiswahili (KS) na Kibukusu (KB) katika mawanda yanayohusu umma katika Kaunti ya Bungoma.

Nafasi ya Lugha za Asili/Mama za Kiafrika

Kwa mujibu wa Mutiga (2005) ugiligili katika sera na upangaji lugha nchini Kenya umefanya lugha za kiasili kubaki nyuma katika kukua na kustawishwa. Tosco (1992), anasisitiza kwamba neno lugha ya asili/mama halitambuliki katika jamii za wingi lugha, kwani ni nadra kupata watoto ambao wanatoka katika familia ambazo zinatumia lugha moja pekee. Kikwazo cha pili ni kwamba, katika

jamii zenye wingi lugha si rahisi kufundisha lugha za kiasili kutokana na ukosefu wa vifaa vya kufundishia (Kapanga, 1998). Hisia za wazazi, walimu na watoto kuhusu lugha wanayofundishiwa na matini yake ndiyo huathiri matumizi ya lugha wanayojifunza. Aidha, kuna utata kuhusu namna ambavyo mafunzo katika elimu ya juu yanavyopaswa kutolewa katika lugha hizi bila kuwa na matarajio ya kuwa na manufaa katika upanuzi wa shughuli za kiuchumi, kiviwanda, na hatimaye kujenga jamii ambayo imeshamiri katika maarifa na teknolojia ya kisasa (Ruiz, 1984). Kulingana na UNESCO (1996), wenzu mzuri wa kufundisha mtoto ni kupitia lugha ya mama. Kisaikolojia, kuna mfumo wa ishara zenye maana akilini mwa mtoto na ndizo ambazo humwezesha kuelewa na kujieleza kijamii. Hii ndiyo njia ya pekee ya mtoto kujitambulisha na wanajamii wenzake. Aidha, katika mfumo rasmi wa elimu, mtoto husika atakuwa na uwezo wa kujifunza kwa urahisi kupita lugha ya mama kuliko jinsi anavyojifunza kupitia lugha asiyofahamu barabara.

Ni dhahiri kuwa kuna baadhi ya lugha za kiasili ambazo hazina othografia, na hali jinsi ilivyo, idadi ya wazungumzaji wa lugha za kiasili inazidi kudhoofika kiasi kwamba KS kimeanza kutumika kama lugha ya kwanza (Githiora, 2002). Sababu mojawapo ni mtindo wa kuchanganya na kubadili msimbo katika mazungumzo. Isitoshe, idadi ya wazungumzaji wa KS inazidi ile ya wanaotumia lugha ya kiasili. Hii ni ithibati tosha kuwa huenda kutokee hali ya mbanduko wa lugha kutokana na jinsi vijana wanaopendelea KS wanavyozidi kupoteza utambulisho wao wa kijamii pamoja na misingi ya utamaduni wao (Massamba, 1986).

Kutokana na hali hii, wapangaji sera wanapasa kutathmini mitazamo ya juu-chini na chini-juu ili kuwe na uhalisia katika utekelezaji wa sera ya lugha (Mazrui na Mazrui, 1993). Katika kiwango hiki ni muhimu kuoanisha masuala ya urazini wa lugha na ustawi wa kitaifa kwa kusisitiza kuhusu matumizi lugha kulingana na mawanda ya uamilifu. Aidha, Prah (2000) anatoa kauli kuwa, ustawi kisayansi na kiteknolojia barani Afrika unaweza kufaulu iwapo lugha za kiasili zitapewa nafasi muhimu katika jitihada zote za maendeleo barani. Nao Webb na Sure (2000) wanashikilia kuwa, umoja-lugha wa kikoloni unapasa kubadilika na kuwa wingi lugha wa Kiafrika.

Uwanja wa Isimu-Jamii

Spolsky (2009) anaeleza kuwa mtazamo wa kijamii wa kuchunguza lugha hutokana na miundo ambayo lugha huibua kulingana na uamilifu wake katika jamii lugha. Akimnukuu Halliday (1978), Khadi anaeleza kuwa lugha huwa na umbo fulani kulingana na mahitaji inayotimiza katika jamii. Kwa mujibu wa Wardhaugh (1987), uwanja wa Isimu-jamii ni maarufu katika kuchanganua mkao wa lugha na jinsi inavyotumiwa na jamii. Kwa vile lugha si ya papo kwa kila mtumiaji lugha au kundi linalotumia lugha fulani, Isimu-jamii huchanganua njia nyingi, na tofauti ambamo lugha huingiliana na jamii (Gumperz & Hymes, 1972). Aidha, jamii nyingi hutumia lugha kwa njia tofauti kutegemea hali na miktadha ya matumizi na kila mtumiaji lugha au kundi la watumiaji lugha hudhihirisha upekee wa aina yake kutegemea mienendo ya kiisimu kama vile uteuzi wa aina za lugha au lugha fulani mahsusi (Otsuji & Pennycook, 2010).

Kwa mujibu wa Wolff (2000), Isimu jamii huchunguza ruwaza za matumizi ya lugha kwa upande mmoja na masuala yanayohusiana na kuwepo kwa tofauti baina ya lugha mbalimbali kwa upande mwingine. Isimu jamii hupania kujibu maswali kama: *ni nani, ipi kwa nani, lini na wapi, kwa nini* na lugha *gani* (Fishman, 1972). Maswali haya yanaakisi masuala muhimu ya kijamii ambayo huibuka pale ambapo watu wawili au zaidi wanaposhiriki katika tukio la mawasiliano kwa kusemezana katika muktadha wa mutagusano wa kijamii ambapo kuna: wahusika, mada, mandhari au miktadha ya kijamii, uamilifu na aina ya lugha.

Kulingana na Spolsky (2007), lugha ina nafasi teule katika mitagusano ya kijamii kutokana na hali kuwa wanajamii lazima washiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Katika hali hii, kuna mitagusano inayowatangamanisha watu katika hafla mbalimbali, na kuna ile inayowaweka kwenye mandhari inayowalazimu kutumia lugha kulingana na miktadha tofauti tofauti. Hata hivyo, inabainika kuwa miktadha ya matumizi ya lugha hutegemea mahali, hali na wahusika, na tatizo lililopo ni kwamba kuna taathira hasi zinazosababishwa na kutengwa kiisimu iwapo wahusika katika tukio la mawasiliano hawafahamu lugha inayotumika katika muktadha husika (Nekvapil, 2006).

Mkao wa Kiisimu-Jamii katika Kaunti ya Bungoma

Matumizi ya lugha katika Kaunti ya Bungoma yanadhihirisha kuwepo kwa mtagusano na mbanduko wa lugha. Miongoni mwa maswala ambayo yamesababisha kuwepo kwa hali hii ni: taathira zinazotokana na utekelezaji wa mfumo wa elimu wa 8-4-4, ukuaji wa miji na viwanda, uhamiaji wa watu, ndoa, hamasa za kisiasa, upanuzi wa miundo misingi na mfufumko wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Kwa mujibu wa Mulokozi (1989), mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa huwa na taathira tofauti tofauti kuhusiana na hali ya kijumla ya mawasiliano, uenezaji wa habari na udumishaji wa ushiriki katika shughuli za maendeleo kijamii, jukumu ambalo kimsingi hutekelezwa na lugha. Hata hivyo, uchangamano wa sera ya lugha (Nevins, 2013), ni mojawapo wa sababu za kutokuwepo kwa uthabiti wa kiisimu hasa katika muktadha wa wingi lugha, hali ambayo hupelekea ugavi wa majukumu na mawanda ya matumizi ya lugha kugemea katika hadhi na taadhima ya lugha (Ogechi, 2003). Ingawa KS kwa sasa ni lugha ambayo imepewa msukumo na serikali katika shughuli mbalimbali za maendeleo (Mukuthuria, 2006), mkao wa kiisimu-jamii katika Kaunti ya Bungoma unadhihirisha uhalisia wa KS na KB kama lugha zenye asili ya Kiafrika zinazomizaniana kiuamilifu katika ugavi wa majukumu.

Lugha ya Kiswahili

Nchini Kenya, KS hutekeleza wajibu muhimu katika mawasiliano baina ya jamii mbalimbali (Mbaabu, 1985), na hivi sasa, lugha hii ina udhibiti na uwezo wa kimatumizi ambao unadhihirika kupitia maenezi yake na mawanda ya kimatumizi. Kwa mujibu wa KS hakimilikiwi na wazungumzaji wenyeji pekee, bali mawanda yake ya kimatumizi yameshamiri katika safu ya kitaifa na kimataifa. Mbali na KS kuwa lugha inayotekeleza majukumu ya kimawasiliano katika viwango vya kitaifa, lugha hii ni lugha rasmi nchini Kenya (Mbaabu, 1996). Kimsingi, kuimarishwa kwake kihadhi ni hatua ambayo imetokana na dhima yake katika miktadha ya kimatumizi, na kutambulika kwake kikatiba (Katiba ya Kenya, 2010). Hata ingawa matumizi ya KS katika mawanda mbalimbali yamezidi kuimarika, suala la haki za lugha ni miongoni mwa

maswala ambayo yanafaa kupewa kipaumbele, na kufaulu kwake kunategemea juhudi za kuzua mikakati inayonua kufufua, kudumisha na kuimarisha matumizi ya KS sawia na lugha zingine za kiasili.

Lugha ya Kibukusu

Furaha, Nyamasyo na Wangia (2016) wanaeleza kuwa KB ni lugha ya Kibantu inayozungumzwa na Wabukusu. Ni lahaja ambayo inakurubiana na takriban lahaja kumi na sita za kabila la Waluhya wanaoishi magharibi mwa Kenya (Heine & Mohling, 1980; & Simiyu, 1985). Ingawa ni lahaja mojawapo ya Kiluhya, kwa minajili ya utafiti huu itachukuliwa kuwa lugha. Idadi kubwa ya wazungumzaji wa KB ni wamiliki wa Kaunti za Bungoma na Trans-Nzoia. Hivyo basi kazi hii inarejelea lugha inayozungumzwa eneo la Kaunti ya Bungoma pekee. KB ni lugha ya kiasili ambayo kwa kipindi kirefu imekuwa ikitumika kama lugha ya kwanza katika eneo hili, huku KS ikiwa lugha ya pili na Kiingereza kama lugha rasmi na ya kufundishia katika uwanja wa elimu (Mulwale, 2008).

Madhumuni

Uamilifu wa lugha katika jamii ni suala tata kwa namna ambavyo kuna mitazamo ya juu-chini na chini-juu kuhusu ni wapi au ni nani anafaa kutumia lugha gani kwa wakati gani. Ili kuwe na uhalisia katika utekelezaji wa sera ya lugha, kazi hii inauia kuchanganua uamilifu wa lugha ya KS na KB kupitia ruwaza za matini zinazodhihirika katika mawanda mbalimbali katika Kaunti ya Bungoma.

MAPITIO YA MAANDISHI

Dhana ya Wingi-Lugha

Kuna vigezo vitatu vinavyotumika kubaini dhana ya wingi-lugha kwa mujibu wa Wei na Moyer (2004). Wingi-lugha kama sifa inayodhihirisha mkao wa kiisimu-jamii katika taifa; mifumo na mipangilio ya wingi-lugha kama asasi katika taifa fulani na wingi lugha wa kibinafsi. Viwango vya wingi-lugha hutegemea masuala ya kijiografia, kihistoria, kitamaduni na kijamii ambapo mataifa mbalimbali huwa na idadi tofauti tofauti za lugha.

Wingi-Lugha wa Kibinafsi

Wingi-lugha wa kibinafsi ni hali ambayo hutokea katika jumua ya lugha nyingi, kwani watu hudhihirisha uwezo wa kuzungumza lugha mbili au zaidi katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano pasi na uzingativu viwango vya umilisi (UNESCO, 1997). Hivyo basi, wingi-lugha wa kibinafsi ni hali ya kijumla inayomizanisha umilisi katika lugha mbili au zaidi, ambapo lugha moja hupendelewa au kuzidhibiti zingine kutegemea mada na miktadha ya mawasiliano miongoni mwa wazungumzaji.

Sifa maalum zinazoambatana na wingi-lugha wa kibinafsi ni uchanganyaji msimbo na ubadilishaji msimbo. Kwa mujibu wa Myers-Scotton (1993), uchanganyaji msimbo ni hali ya kuchanganya lugha au zaidi katika muktadha sawa wa usemi au wa kidiskosi, huku ubadilishaji msimbo ni mkakati unaotumiwa na mjozilugha kwa lengo kujitambulisha na kundi linalotumia lugha fulani mbali na zile lugha zingine ambazo ana umilisi kwazo. Kazi hii inabaini miktadha ambamo hali hii ya wingi lugha wa kibinafsi hutokea kati ya KB na KS katika Kaunti ya Bungoma.

Wingi-Lugha Kiasasi

Halliday (1978, 1985) anaeleza kuwa lugha hutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii, hususan katika miktadha ya wingi-lugha, ambapo lugha hupewa hadhi kisheria ili zitumuke katika asasi za kijamii zinazohitaji matumizi ya lugha kadhaa kutegemea mawanda hali inayopelekea kuwepo kwa wingi-lugha kiasasi. Wingi-lugha kiasasi hurejelea jamii au mataifa ambayo yametengea majukumu maalum lugha fulani kupitia amri au sheria kikatiba pasi na uzingativu kuhusu utekelezaji au kutumika na raia. Aidha, wingi-lugha kiasasi unaweza kujumlisha hali zote ambazo asasi tofauti tofauti hujitambulisha na lugha fulani maalum hasa katika nyanja za elimu, dini na mawasiliano ya kimataifa. Hivyo basi jamii au mataifa yanaweza kuainishwa kulingana na hadhi ya lugha kisheria pamoja na idadi ya lugha zinazozungumzwa katika mipaka yake kwa kuangazia majukumu yanayotekelezwa na lugha hizo. Kazi hii inashughulikia mawanda ambayo hayana sharia rasmi zilizowekwa za matumizi ya lugha kama vile sokoni, kanisani na utawala ili kuchunguza namna lugha ya KS na KB zinavyokamilishana kiuamilifu.

Daiglosia

Mfumo wa matumizi ya lugha katika jamii za wingi-lugha huakisi hali ya uteuzi wa lugha kwa misingi ya kiuamilifu na kuna manufaa ya kutumia lugha mbalimbali au aina tofauti tofauti za lugha kwa minajili ya kutimiza majukumu mbalimbali. Kwa mujibu wa Ferguson (1959), dhana daiglosia hurejelea hali ya matumizi ya lugha kutegemea majukumu ama ya hadhi ya juu au ya hadhi ya chini na ambayo yanatekelezwa na lugha tofauti tofauti katika jamii maalum. Anaonyesha kwa mfano namna miktadha kama vile ya mahubiri ya kidini, mihadhara ya vyuo vikuu au magazeti ingetumia lugha ya hadhi ya juu ilhali mazungumzo ya kawaida katika familia au kati ya marafiki ingetumia ile ya hadhi ya chini. Mtazamo huu unatathmini jinsi hali hii inavyochangia katika kudhoofika au kuimarika kwa KS na KB kiuamilifu katika mazingira yenye wingi lugha.

Katika muktadha wa wingi lugha kuna uwezekano wa kuwa na daiglosia ‘thabiti’ na ‘isiyo-thabiti’ (Brenzinger, 2007). Katika mazingira kama haya, ni vigumu lugha kuwa na lugha ambazo zina hadhi sawa hasa kwa kukadiria vipimo vya matumizi, viwango vya ustadi kiumilisi, taadhima na uamilifu. Miktadha kama hii huelekeza lugha zilizo na udhibiti wa kiisimu kudhalilisha zile zisizo na udhibiti, hali ambayo husababisha tukio la ama mbanduko wa lugha au lugha kudhoofika kiasi cha kutoweka.

Mbanduko wa Lugha

Kudidimia kwa lugha kiuamilifu huambatana na sifa dhahiri zinazodhihirisha jinsi lugha zinavyopoteza majukumu yake ya kimawasiliano kiasi kwamba vizazi vinavyofuatia kutoibwia lugha mama/asili kama lugha ya kwanza. Utafiti mwingi umefanywa kuhusu kudidimia kwa matumizi ya lugha hafifu kutokana na udukizi wa lugha babe. Mbaabu (1996) anahoji kuwa, Bara la Afrika lina lugha nyingi isipokuwa zinazotumika ni chache hasa kwa kuzingatia idadi ya wazungumzaji pamoja na hali ya uthabiti wa kiisimu unaozilinganisha na kuziorodhesha lugha hizo kiuamilifu. Kuna pale ambapo lugha hupata wazungumzaji huku zingine zikipoteza kutokana na sababu kama vile lugha inayopoteza wazungumzaji kutokana na uchakavu wa lugha kiasi cha kutoweka. Kulingana na Batibo (2005), lugha zilizo na idadi ndogo ya

wazungumzaji hukumbwa na hatari ya kuangamia. Aidha, kuna pale ambapo watu hutupilia mbali matumizi ya lugha fulani kwa hiari au kwa kulazimishwa. Mchakato mzima wa watu kubadili matumizi ya lugha na kuchukua lugha nyingine hujulikana kama mbanduko wa lugha.

Mbanduko wa lugha ni mojawapo ya vipengele vinavyopambanua dhana nzima ya mabadiliko ya lugha. Kwa mujibu wa Aitchinson (1991), mabadiliko katika lugha yapo na huathiri uamilifu pamoja na muundo wa lugha. Mbanduko wa lugha ni pale wazawa wa lugha wanapojitenga na lugha yao na badala yake kuhamishia utiifu wao wa kimawasiliano kwa lugha nyingine iliyo na udhibiti.

Miongoni mwa visababishi vya mbanduko wa lugha ni kama vile: uhamiaji kutoka maeneo ya vijijini hadi mijini, ustawi wa kijamii, pamoja na jumla ya masuala yanayoambatana na athari za ujozilugha na daiglosia. Kwa mujibu wa Dorian (1998), wazungumzaji wanaweza kutupilia mbali matumizi ya lugha yao na kupendelea lugha nyingine kutokana na manufaa ya kijamii na kiuchumi. Katika muktadha huu, lugha ambazo zina uthabiti kiuchumi na kijamii ndizo hujiimarisha katika mawanda mengi ya kiuamilifu na hivyo idadi ya wazungumzaji huzidi kuongezeka.

Uamilifu wa KS na KB

Kaunti ya Bungoma ni kielelezo cha changamoto ambazo ni dhahiri, na zinazoakisi namna utekelezaji wa mfumo mpya wa ugatuzi nchini Kenya unavyotarajiwa kukabiliana na mitazamo ya kijamii inayodhihirisha upendeleo wa lugha fulani kutokana na dhima yake, huku mingine ikidhihirisha kauli kuwa watu hujieleza vyema katika lugha zao za kiasili (UNESCO, 2003). Kulingana na Batibo (2005), mataifa mengi barani Afrika yana mpangilio wa traiglosia ambapo lugha za kikoloni ndizo zenye hadhi ya juu na hutekeleza majukumu rasmi, lugha za kieneo ambazo ni za kimtagusano baina ya makundi mbalimbali ya kijamii na lugha asili ambazo hutekeleza majukumu ya hadhi ya chini. Katika Kaunti ya Bungoma, hali inayojitokeza ni mifumo miwili ya ujozi lugha na daiglosia ambapo KS na KB zinashindana. Kulingana na Sebba (2011), hali ya ujozi lugha unaoenda sambamba na daiglosia husababisha hali lugha husika kutumika lakini zikiwa zimetenganishwa kutegemea majukumu

zinazotekeleza. Hali hii inasheheni ugiligili wa kiutendeti na wa kimtazamo unaodhihirisha uegemezi wa kimatumizi kwa upande wa KS ikilinganishwa na KB.

Hata hivyo, msimamo wa kikatiba kuhusu lugha ni fursa kwa wadau wote katika ngazi za kijamii kutambua Kiswahili na Kibukusu kama kiungo muhimu cha kuimarisha na kudumisha usimamizi bora katika asasi mbalimbali za serikali na za umma, kwa vile hii ni hatua muhimu inayofanikisha viwango vya ubora katika ugavi wa rasilimali za kimsingi na huduma muhimu. Aidha, pana haja ya kuzindua nyenzo za kuzipa lugha za kiasili hususan Kibukusu msukumo wa 'kimatumizi' kupitia miktadha rasmi na ya kijamii (Brenzinger, 2007), ili kiweze kutimiza majukumu yake ya kimawasiliano katika kiwango cha Kaunti hasa maeneo ya mashinani, na ambayo yanazidi kunyakuliwa na KS; na namna ambavyo Kibukusu kinaweza kukabiliana na nguvu dukizi zinazotokana na kuidhinishwa kikatiba kwa KS lugha rasmi nchini Kenya.

Kulingana na Nuyts (1989), uamilifu wa lugha ni jumla ya nyenzo zinazoiwezesha lugha kuhimili na kutimiza majukumu mbalimbali kulingana na matarajio ya mtumiaji lugha katika jumua lugha husika. Mbali na kuchanganua misingi ya dhana ya uamilifu na aina zake, Nuyts anachunguza uhusiano baina ya majukumu yatekelezwayo na lugha na dhima ya mawasiliano kijumla. Hata hivyo, kuna mianya kuhusu jinsi ambavyo ruwaza mbali mbali zinabaini uamilifu wa lugha mintarafu ya kanuni za dhana yenyewe ya uamilifu, muktadha na uanishaji wake. Inabainika kuwa ruwaza za uteuzi wa lugha na uamilifu wake huwa na upekee kwa kila lugha. Kama anavyodai Romaine (2006), uamilifu ni kigezo cha kimsingi katika mifanyiko ya kimfumo inayojumuisha vipashio katika mfumo maalumu wa kiisimu kwa upande mmoja, na utendaji kazi wa lugha kwa upande mwingine. Hivyo basi, uamilifu wa KS na KB unapasa kudhihirika katika mfumo wa kijamii kutokana na namna ambavyo jamii hutegemea lugha kama wenzu wa mtagusano unaowezesha lugha kutumika katika kutimiza mahitaji mbalimbali ya kimawasiliano kwa njia adilifu na ya haki.

Uamilifu na uteuzi wa lugha hukamilishana, kwani hali hizi hudhihirisha umaalum katika utambuzi wa

miktadha ambamo lugha hutumika. Yeh, Chan na Cheng (2004) wanabaini mitazamo ambayo inafafanua uteuzi wa lugha. Mwanzo, kuna mtazamo wa kijamii ambao huangazia hali ya kuratibisha makundi ya watu kulingana na mwenendo wao wa kuteua lugha. Pili, kuna mtazamo wa kijamii-nafsia ambao hutoa sababu za kibinafsi kutegemea mahitaji na haiba ya mtu binafsi katika kueleza sababu za kuteua lugha fulani, na kisha kuna ule mtazamo wa kiantropolojia ambao huangazia maswala kama vile mfumo wa maadili ya kijamii na utamaduni kama wenzu wa kueleza na kubashiri uteuzi wa lugha miongoni mwa makundi fulani ya watu. Kwa upande mwingine, Huang (1988) na Graddol (1997) wanapambanua maswala ya kijamii ambayo huelekeza watu kuteua lugha fulani. Kulingana na maoni yao; umri, elimu, uana, hadhi na taadhima pamoja na makazi huathiri pakubwa mitazamo ya wenyeji kuhusu uamilifu wa lugha na hadhi halisi ya lugha, kwani hivi ndivyo vigezo vinavyoleta wiano kati ya lugha na utambulisho wa kijamii. Pale ambapo lugha fulani haina uwezo wa kukimu mahitaji muhimu ya kimawasiliano, kuna haja ya jamii husika kuteua lugha yenye uwezo zaidi. Hata hivyo uteuzi huo haupaswi kuhitilafiana na mawanda yote ya uamilifu wa lugha. Kutokana na msingi huu, inabainika kuwa uteuzi wa lugha hutegemea sifa za kimsingi za watu katika jamii.

NADHARIA YA UTAFITI

Uwanja wa sera na mipango ya lugha unahusishwa na kazi za awali za Ferguson (1959), Das Gupta (1968), Fishman (1972, 1974, 1983), Haugen (1972) miongoni mwa wengine miaka ya 1960 na 1970. Kaplan (2003), Ricento (2000) na Nekvapil (2011) wanaeleza kuwa maswala mengi kuhusu sera za lugha yaliendelezwa baada ya kutengana kwa mataifa mbalimbali na watawala wao wa kikoloni, baada ya vita vya pili vya Ulimwengu. Mataifa mapya Afrika, Kusini na Kusini Mashariki mwa Asia yaliibuka. Mataifa haya yalisababisha kuwepo kwa haja ya kuwa na lugha moja ya taifa ya kuwaunganisha wananchi. Aidha, lugha hiyo ingesababisha mabadiliko ya kisiasa na kijamii yanayofaa. Miundo ya kijamii na kiutamaduni inayohimiza umoja hupunguza tofauti za kiuchumi na hata nafasi za kupata elimu.

Asili ya mitazamo ya kimapokeo ya mpango wa lugha yenye mizizi yake kwenye usasa, iliasisiwa kupitia kazi ya Haugen (1983). Alieleza hatua nne za miundo ambayo iliendelezwa na wanaisimu jamii wa baadaye kama vile Kaplan na Baldauf (1997, 2005). Walieleza miundo ya upangaji lugha kama vile; mpangilio kulingana na hali ya kijamii, hali ya lugha yenyewe, mipango ya lugha katika elimu (Cooper, 1989) na mipango kuhusu taswira zitokanazo na hadhi ya wapokezi (Ager, 2005). Ferguson (1977) anaeleza kuwa shughuli zote za mipango ya lugha hufanyika katika muktadha fulani wa kiisimu jamii. Anaendelea kusema kuwa hali na upeo wa mpango huo unaweza tu kueleweka kwa kina kutegemea muktadha huo huo. Anasisitiza kuwa muktadha wa kiisimu jamii ufasiriwe kuhusisha hali zote zinazoathiri ikolojia ya lugha na idiolojia au juhudi za kuingilia katika kutumia lugha.

Naye Spolsky (2004, 2009) anafafanua sera ya lugha ambayo anaitambua pia kama Usimamizi wa lugha, huhusu uchaguzi ambao huwa na vipengele vitatu; uamilifu wa lugha, idiolojia au imani zinazohusiana na lugha pamoja na usimamizi wa uamilifu wa lugha. Anajadili kuwa uchaguzi wa sauti fulani, au maelezo fulani au aina fulani ya lugha ni uamuzi ambao hufanywa kila mara na watu binafsi, makundi fulani ya watu au makundi yenye mamlaka fulani katika miktadha fulani ya kijamii. Muundo wa usimamizi wa lugha ulioelezwa na Spolsky unafafanua uchaguzi wa lugha kwa kuzingatia misukumo ya dhati inayotokana na uamilifu wa lugha, imani kuhususiana na lugha hiyo na usimamizi wa lugha kwa kuzingatia mawanda ya lugha yenyewe. Utafiti huu unatumia misingi ya muundo wa usimamizi wa lugha ulioendelezwa na Spolsky (2004, 2009) ambaye anazingatia moja kwa moja namna lugha inavyotumiwa katika mawanda mbalimbali na wala sio kinachofikiriwa kutendeka au kile kinachopangwa na wengine kuwa kifanyike.

Usimamizi wa Lugha

Spolsky (2004) anaeleza kuwa usimamizi wa lugha ni tendo la watu binafsi au makundi ya watu kuamua uamilifu wa lugha. Hili linaweza kutekelezwa katika viwango tofauti katika jamii. Kutoka kwa viongozi wenye mamlaka ya kutunga sheria kwenye kiwango cha makro hadi kiwango cha watu binafsi katika jamii kuteua lugha watakayoitumia katika

kiwango cha mikro. Yaani miundo ya juu-chini au chini-juu mtawalia. Shohamy (2006) anaeleza kuwa lugha haina mipaka. Watu binafsi au makundi ya watu hutaka kuidhibiti na kuiendesha ili kuhimiza idiolojia zao za kisiasa, kijamii, kiuchumi na hata kibinafsi. Anaendelea kusema kuwa katika muundo wa juu – chini usimamizi wa lugha hutekelezwa kwa jaribio la kuathiri imani na uamilifu wa lugha ili kuafikia malengo fulani.

Aidha, Cooper (1989) akiangazia suala hili la usimamizi wa lugha anaeleza namna wanaohusika huathiri tabia gani, kwa watu gani, kwa hatima ipi, kwa utaratibu gani na matokeo yepi. Hadhi ya lugha huhusika zaidi na nafasi ya lugha kutegemea mawanda inamotumika na ujifunzaji wa lugha huhusika hasa sera la lugha katika elimu.

Spolsky (2009) anafafanua usimamizi wa lugha kwa kuchunguza uamilifu wake katika mawanda mbalimbali. Utaratibu wa sera ya lugha huwa tofauti katika miktadha tofauti ya kijamii na idiolojia za lugha hizo hutofautiana kulingana na mawanda inamotumika.

Ikolojia ya Lugha

Mwelekeo wa ikolojia ya lugha ulizinduliwa na Einar Haugen (1972), na umefasiliwa kama uchunguzi kuhusu mwingiliano baina ya lugha na mazingira, ambapo mazingira kamili ya lugha ni jamii ambayo hutumia lugha kama mojawapo wa msimbo wake. Kwa mujibu wa Martin (2003), mtagusano kati ya lugha na mazingira zinakozungumzwa lugha hizo hudhihirisha uhusiano wa kutegemeana. Uhusiano huu hutambulika kupitia mifumo ya kijamii inayoambatana na miktadha halisi ya kijamii, kisiasa na kihistoria ambamo lugha hutumika. Kulingana na Skutnabb-Kangas na Harmon (2018), mazingira halisi ni kigezo cha kimsingi kinachobaini uhusiano dhahiri uliopo baina ya lugha mbalimbali na wazungumzaji wa lugha hizo.

Kanuni ya kimsingi ya dhana ya ikolojia ya lugha kwa mujibu wa Haugen ni kwamba, lugha hutegemea mazingira inamotumika, na huhifadhiwa akilini mwa watumiaji wa lugha husika. Kwa vile lugha ni kiungo muhimu kinachowaweka pamoja watumiaji lugha husika, mazingira ya kijamii na yale halisi yana umuhimu mkubwa katika kuelekeza mkondo wa matumizi ya lugha katika jamii husika.

Dhana ya Ikolojia ya Lugha vilevile inakariri kuhusu dhima ya utambuzi kuhusu uhai wa lugha, malengo pamoja na miundo yake kama msingi wa ukuzaji, udumishaji na uhifadhi wa lugha (Bastardas-Baoda, 2002). Dhana hii inapambanua jinsi lugha zinavyozuka na kutagusana katika mfumo hai na ambao unadhihirisha kanuni za mtagusano wa lugha katika miktadha ya kijamii, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi.

Province na Kretzer (2018) wanaeleza kuwa kipengele cha Ikolojia ya Lugha huhusu maamuzi ya uchaguzi wote wa kiisimu ambao hufanywa na watu au kundi la watu. Kutokana na msingi huu, dhana ya ikolojia ya lugha ni uchunguzi wa kimseto katika miktadha maalum ya kijamii na kisiasa, ambapo hali mbalimbali kuhusu lugha hubuni, huakisi na huchambua mifumo na mamlaka mbalimbali. Mitazamo kuhusu ikolojia ya lugha imeelekeza utafiti huu kuchanganua mtagusano wa lugha na athari zake katika Kaunti ya Bungoma. Masuala ya uchanganyaji na ubadilishaji wa msimbo kati ya KS na KB yatachanganyuliwa na kuelezwa namna yanavyotokea katika mawanda mbalimbali ya uamilifu wa lugha hizi.


Aidha, muundo wa uchunguzi wa lugha unaohusisha jamii hujikita katika uamilifu wake (Halliday, 1985 ; Martin, 1997 ; 2000 ; 2001). Hawa wataalamu wanaafikiana kuwa, lugha huwa jinsi ilivyo kwa sababu ya majukumu ambayo inafaa kutimiza. Tangu au ruwaza za matini zinazoibuka katika mitagusano ya kijamii huwa na miundo teule inayoweza utimizaji wa malengo yake. Biber (1988, 2006) anabainisha mitazamo mitano ya kueleza ruwaza za matini, kama vile usimulizi, maelezo, ombi/rai, mahojiano na ufafanuzi. Naye Paltridge (2001) anaeleza ruwaza za matini kuwa miundo ya namna usemi hupangwa na hujitokeza kwa tangu kama vile maelezo, masimulizi, maagizo, ufafanuzi, na baadaye akahusisha pia barua, hadithi na matangazo. Knapp na Watkins (1994) nao wanaeleza utanzu kuwa michakato ya lugha kama vile kueleza, kufafanua, kujadili ilhali ruwaza za matini kuwa matokeo yake kama vile ripoti, hadithi na maonyesho. Katika kazi hii kwenye ikolojia ya lugha michakato ya lugha inayounda aina mbalimbali za matini zitabainishwa na kutumiwa kueleza namna lugha ya KS na KB zinavyotangamana katika uamilifu wa kijamii. Michakato hiyo ni pamoja na maswali na majibu,

maelezo, masimulizi, mahojiano/majadiliano, mahubiri na hotuba.

Hata hivyo, Spolsky (2004) anafafanua kuwa sera ya lugha halisi ya jamii hupatikana kwenye uamilifu wake katika mawanda ya kijamii. Hivyo basi, matumizi yake namna yanavyoelezwa kwenye sheria kama vile katiba za nchi haidhihirishi hali halisi ya lugha. Ni muhimu kutambua kuwa baadhi

ya lugha huonekana kuenea zaidi kutokana na sababu mbalimbali namna inavyobainika katika uamilifu kati ya KB na KS katika Kaunti ya Bungoma.

Muundo ufuatao ni muhtasari wa nadharia ya sera ya lugha inavyofafanuliwa na Spolsky (2004, 2009) na unawasilishwa kwa namna ambavyo umetumiwa kueleza kazi hii ;



Utaratibu wa Sera ya lugha kwa misingi ya Spolsky (2004, 2009) Pamoja na ruwaza za matini Paltridge (2001)

Asili : Kutokana na Province na Kretzer (2018) na Paltridge (2001)

MBINU ZA UTAFITI

Muundo mseto ndio uliongoza utafiti huu. Utafiti wa maktaba na wa nyanjani ulifanywa kwa kuzingatia kanuni za muundo wa kimaelezo na kiupelelezi katika kukusanya, kuchambua, kuchanganua pamoja na kuwasilisha matokeo ya

utafiti. Kwa mujibu wa Salkind (2010), Mallinson (2013) na Babbie (2007), muundo wa kimaelezo na kiupelelezi ni mwafaka katika uchunguzi huu kwa vile unafafanua na kutalii miktadha maalum na ya kijumla kuhusu uamilifu wa Kiswahili na Kibukusu katika Kaunti ya Bungoma. Aidha, data ya iktisadi ilitumiwa kuyapa uzito maelezo kwa kuangalia ruwaza za matumizi ya lugha ya KB, KS na KS/KB katika mawanda yasiyo rasmi yaliyoteuliwa.

Utafiti ulitumia usampulishaji dhamirifu kwa kuzingatia muktadha wa biashara, Kanisani na utawala hasa kupitia baraza la Chifu. Kulingana na Morgan (2008), mbinu hii ya kusampuli huchangia katika kupata data zinazotokana na mfumo mpana wa ushirikiano miongoni mwa wahusika, na ni faafu katika kupata data miongoni mwa wazungumzaji wa KS na KB ambao idadi kamili si rahisi kujulikana (Rowland & Flint, 2004).

Uchunzaji usio-shirikishi ulitumika kwa kuongozwa na kifaa cha kudondoa data. Uchunzaji usio-shirikishi ulizingatia mandhari na miktadha maalum ya mitagusano ya lugha, ambapo hoja muhimu zilinukuliwa kutokana uhalisia wa matukio katika maeneo ya nyanjani; kanisani, sokoni na katika mikutano ya baraza la Chifu. Data ilipangwa, kuchanganuliwa na kuelezwa ili kuwasilisha uhalisia wa uamilifu wa lugha hizi mbili licha ya sera ya lugha kufafanuliwa katika katiba ya Kenya (2010).

Isitoshe, kanuni za maadili zilizingatiwa katika hatua zote, kwa kuhakikisha kwamba washiriki wanapewa haki na heshima katika misimamo yao ya kitamaduni, kitabaka, kidini, kijinsia na hata kiumri. Utafiti ulitii kanuni za usiri, uhifadhi wa taarifa binafsi, uwajibikaji, pamoja na uzingativu wa usayansi katika utekelezaji na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Aidha, ridhaa ya kushiriki katika utafiti iliombwa kutoka kwa asasi husika.

Jedwali 1:

| Mawanda | Wahusika | Mandhari |
|----------|---|---|
| Biashara | Wafanyibiashara, wahudumu na wateja | Sokoni, Madukani, burudani |
| Dini | Kasisi, mhubiri, walimu wa dini | kanisani |
| Utawala | Chifu, Afisa wa polisi, Naibu wa Chifu, Gavana, Naibu wa Gavana | Stesheni, Afisi ya chifu, Ukumbi wa baraza la Chifu, Ukumbi wa Umma |

MATOKEO NA MJADALA WA UTAFITI

Katika kueleza mhimili wa Usimamizi ulivyoelezwa na Spolsky (2004) maoni ya Fishman (1972) ya dhana ya uchanganuzi wa mawanda imezingatiwa. Yaani nani hutumia lugha ipi katika mawanda yapi? Kimsingi, dhana hii inabaini mawanda ya uamilifu wa lugha kwa kuzingatia mzungumzaji, mahali na mada.

Katika jumua lugha, wazungumzaji ama hutumia aina tofauti tofauti za lugha moja katika mawanda mbalimbali, au huteua lugha faafu kutegemea mawanda ya matumizi ya lugha hususan katika miktadha ya wingi lugha. Aidha, uteuzi wa lugha au lahaja faafu hutegemea masuala kama vile tabaka, hadhi, urasmi na dhima, hata kama mada ni ile ile. Hali ya wingi lugha na utofauti wa lugha huwaelekeza watumiaji lugha kutumia lugha kutokana na kauli za kimtazamo na kiuteuzi.

Mandhari na miktadha tofauti tofauti ambamo lugha hutumiwa huzingatwa kutegemea michakato na ruwaza za kiisimu katika jumua lugha husika. Katika mtazamo huu, Fishman (1972) ameorodhesha mawanda ya matumizi ya lugha kwa misingi ya mandhari kama vile, nyumbani, barabarani, darasani, dukani, chuoni, kazini, michezoni pamoja na katika asasi za kidini na vyombo vya habari, ambapo kila mojawapo ya mawanda haya hudhihirisha sifa bainifu za kiisimu. Katika utafiti huu mawanda yaliyoteuliwa ni yale yasiyo rasmi kama vile dini, mikutano ya utawala unaohusisha umma kwenye baraza la chifu, mikutano ya kushirikisha maoni ya umma kwa masuala mbalimbali ya kijamii na au mikutano ya ofisi ya Gavana pamoja na biashara mbalimbali inavyowasilishwa katika jedwali lifuatalo ;

Kwa kurejelea mawanda haya, ilibainika kuwa KS, mbalimbali inavyowasilishwa katika jedwali KB na KS/KB zilitumika kwa kuzingatia ruwaza lifuatalo;

Jedwali 2:

| Mawanda | Ruwaza Ya Matini {n(%)} | | | | | |
|-----------------|-------------------------|------------|------------|---------------------------|------------|-----------|
| | Maswali/majibu | Masimulizi | Maelezo | Mahojiano/ Majadiliano | Mahubiri | Hotuba |
| Biashara | | | | | | |
| • KS | 08 (26.67) | | 05 (16.67) | 05 (16.67) | | |
| • KB | 12 (40.0) | | 10 (33.33) | 08 (26.67) | | |
| • KS/KB | 10 (33.33) | | 15 (50%) | 17 (56.67) | | |
| Dini | | | | | | |
| • KS | 06 (20.0) | 04 (13.33) | 02 (6.67) | | 04 (13.33) | |
| • KB | 08 (26.67) | 05(16.67) | 04 (13.33) | | 06 (20.0) | |
| • KS/KB | 16 (53.33) | 31 (70.0) | 24(80) | | 20 (66.67) | |
| Utawala | | | | | | |
| • KS | 10 (33.33) | 02 (6.67) | 03 (10.0) | 03 (10.0) | | 18 (60.0) |
| • KB | 08 (26.67) | 13 (43.33) | 10 (33.33) | 07 (23.33) | | 02(6.67) |
| • KS/KB | 12 (40.0) | 15 (50.0) | 17 (56.67) | 20 (66.67) | | 10(33.33) |

Mawanda ya Biashara

Ilibainika kuwa ruwaza ya maswali na majibu, maelezo, mahojiano/majadiliano ndiyo iliyodhihirika. Aghalabu jibu la swali lilitolewa kwa lugha iliyotumiwa kuuliza swali. Aidha,

Lugha ya KB (40%) ilitumiwa zaidi katika ruwaza hii kuliko KS (26.67%) au KS/KB (33.33%). Wakati majadiliano yamechacha moto, kiwango cha kuchanganya msimbo kati ya KS na KB yanakuwa juu (56.7%) ikifuatiwa na KB (26.67%) kisha KS (16.67%). Isitoshe, Katika ruwaza ya maelezo, KS/KB ilibainika zaidi (50%), KB (33.33%) na KS (16.67%).

Mawanda ya Dini

Katika mawanda ya dini, ruwaza ya mahubiri ilionekana kutawala mawanda haya. Kulikuwepo na hali za kubadili na kuchanganya msimbo KS/KB (66.67%), KB (20%) na KS (13.33%). Uchanganyaji msimbo ulibainika zaidi wakati ambapo mahubiri pamoja na washiriki wengine walipokosa neno mwafaka la papo hapo la kufafanua waliyoyazungumzia. Maswala yaliyoonekana kuteka hisia zaidi yalifafanuliwa kwa lugha ya KB. Lugha ya KS ilionekana

kutumiwa kwa uchache mno ikilinganishwa na KB katika ruwaza zote.

Mawanda ya Utawala

Mawanda haya yalikusishwa zaidi mikutano katika baraza la chifu, mikutano ya Gavana wa Kaunti ya Bungoma pamoja mikutano iliyoshirikisha umma katika kutoa maoni kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu uongozi na jamii yote kwa jumla. Ruwaza ya hotuba ilionekana kutumiwa kwa wingi huku asilimia kubwa ikitolewa kwa lugha ya KS (60%). Hili ni dhahirisho kuwa mikutano ya utawala ilizingatia sera ya lugha ya Kitaifa ambayo ilihimiza matumizi ya lugha ya KS ambayo sio tu lugha ya taifa bali pia ni lugha rasmi (Katiba, 2010). Maswali na majibu yaliwasilishwa zaidi kwa kubadili na kuchanganya msimbo kwa namna mbalimbali (40%).

Katika mawanda yote matatu, ilibainika kuwa ya hali ya KS/KB ilitokea zaidi wakati wa maamkuzi au wakati wa kuanza na au wakati wa kubadilisha mada ya mazungumzo. Maneno ya kuunganisha kama vile *halafu, labda, si, na au* yalitumiwa huku yakipewa toni ya lugha ya KB.

Wakati mwingine sentensi husemwa kwa lugha ya KS kisha yale ya KB huchopekwa na vile vile kwa

lugha ya KB kisha ya KS huchopekwa. Ujumuishaji wa kubadili au kuchanganya msimbo ulidhihirisha zaidi wepesi katika kuwasiliana. Sentensi kamili za KB zilidhihirika zaidi wakati wa kujadiliana masuala ya kihisia na yenye kuzozana au kuibua kutoelewana. Aidha, maswala yaliyohusiana moja kwa moja na mazingira yao pamoja na utamaduni yalijadiliwa kwa lugha ya KB bila ugumu wowote.

HITIMISHO

Kazi hii inadhihirisha namna ambavyo KS na KB zinavyotangamana na kushirikiana katika mawanda mbalimbali katika Kaunti ya Bungoma. Uamilifu wa lugha katika jamii huweza kuelezwa tu kwa ukamilifu kwa kurejelea matumizi halisi katika jamii na wala sio sera za lugha za nchi. Aidha muundo wa nadharia wa Spolsky hauwezi kuelezwa kwa upekee pasipo kuhusisha ruwaza mbalimbali ilivyoelezwa na Paltridge (2001). Uteuzi wa lugha kati ya washiriki ulichangiwa pia na ruwaza ya matumizi ya lugha. KS na KB ni lugha ambazo zina kamilishana na kuathiriana kiuamilifu.

MAREJELEO

- Aitchison, J. (1991). *Language Change: Progress or Decay* (2nd ed.). Cambridge: Cambridge University Press.
- Babbie, E. (2007). *The Practice of Social research*. Belmont CA: Thompson-Wadsworth. (pg. 87-89)
- Baldauf, R. B. (2005). Language Planning and Policy Research: An overview. In E. Hinkel (Ed.), *Handbook of Research in Second Language Teaching and Learning* (pp. 957–970). Mahwah, NJ: Lawrence Erlbaum Associates. <https://doi.org/10.1080/14664208.2016.1129477>
- Bastardas-Boada, A. (2002). Language Planning and Language Ecology : Towards a theoretical integration, scribd.com. [Http://www.scribd.com/doc/3025205/Language-Planning-and-Language-Ecology-Towards-a-theoretical-integration](http://www.scribd.com/doc/3025205/Language-Planning-and-Language-Ecology-Towards-a-theoretical-integration). 10. 02. 2022
- Batibo H. M. (2005). *Language Decline and Death in Africa: Causes, Consequences and Challenges*. Clevedon: Multilingual Matters.
- Batibo H. M. (1997). “The fate of minority languages of Botswana,” Katika B. Smeija na M. Tasch (wh.) *Human contact through language and linguistics*. (uk. 243-5). Frankfurt: Peter Lang.
- Biber, D. (1988). *Variation across Speech and Writing*. New York, NY: Cambridge University Press. <https://doi.org/10.1017/CBO9780511621024>
- Brenzinger, M. (mh.) (2007). *Language Diversity Endangered*. Berlin: Mouton de Gruyter.
- Cooper, R. L. (1989). *Language Planning and Social Change*. Cambridge, Cambridge University Press.
- Das Gupta, J. (1968). Language Diversity and National Development. *Language Problems of Developing Nations*, 17-26.
- Dorian, N. (1998). Western language ideologies and small-language prospects. In L. Grenoble & L. Whaley (Eds.), *Endangered Languages: Language Loss and Community Response* (pp. 3-21). Cambridge: Cambridge University Press. doi:10.1017/CBO9781139166959.002
- Fishman, J. (2006). *Do not leave your language alone: The hidden status agendas within corpus planning in Language Policy*. Mahwah NJ: Multilingual Matters Ltd.
- Fishman, J. (1991). *Reversing Language Shift: Theoretical and Empirical Foundations of Assistance to Threatened Languages*. New York: Multilingual Matters.
- Fishman, J. A. (1974). Language planning and language planning research: The state of the Art. In J. A. Fishman (Ed.), *Advances in language planning* (pp. 15–33). The Hague: Mouton.
- Fishman, J. (1972). “Domains and the Relationships between Micro- and Macro-Sociolinguistics.” Katika J.J. Gumperz & D. Hymes (wh), *Directions in Sociolinguistics: Ethnography of Communication*. New York: Academic Press. uk. 435-453.
- Furaha, M. M., Nyamasyo, E. A. & Wangia, J. I. (2016). *The other side of the Coin: Borrowing*

- and Vitality in Lubukusu. *International Journal of Humanities and Social Sciences. Vol.10 (2)*
- Githiora, C (2002). “Sheng: Peer Language, Swahili dialect or emerging Creole?” *Journal of African cultural studies. 15:* uk. 159-193.
- Graddol, D. (1997). *The future of English?* London: British Council.
- Halliday, M. A. K. (1978): *Language as a social Semiotic: the social interpretation of Language and Meaning.* London: Edward Arnold.
- Haugen, E. (1972). *The Ecology of Language.* Stanford, CA: Stanford University Press.
- Huang, S. (1988). A Sociolinguistic Profile of Taipei, In Chen na Huang The Structure of Taiwanese: A Modern Synthesis (uk. 301-335). Taipei: The Crane Publishers.
- Heine, B. & Mohling, W. J. C. (1980) *Language and Dialect Atlas of Kenya.* Berlin: Dietrich Reimer Verlag, Vol. 1.
- Kapanga, A. (1998). “Impact of language variation and accommodation theory on language maintenance? An Analysis of Shaba Swahili.” Katika L. A. Grenoble & L. J. Whaley (wr). *Endangered languages: Current issues and future prospects.* (uk. 134-149), Cambridge University Press.
- Kaplan, C. D, Korf D. & Sterk C. (1987). “Temporal and social contexts of heroin-using populations an illustration of the snowball sampling technique.” *The Journal of nervous and mental disease, 175(9):* uk. 566-574.
- Kaplan, R. B. & Baldauf, R. B. (1997): *Language Planning from Practice to theory.* Clevedon: Multilingual Matters.
- Knapp, P., & Watkins, M. (1994). Context-text-grammar: Teaching the genres and grammar of school writing in infants and primary classrooms. Text productions.
- Lu, L. (1988). “A Survey of Language attitudes, Language use and Ethnic Identity in Taiwan.” Fu Jen Catholic University.
- Mallinson, C. (2013). *Data collection in sociolinguistics: Methods and Application.* Newyork: Routledge.
- Martin, J. R. (1997). *Analysing genre: Functional parameters.* In F. Christie & J.R. Martin (Eds.), *Genres and institutions: Social processes in the workplace and school* (Uk. 3-39). Cassell.
- Martin, J. R. (2000). *Grammar meets genre: Reflections on the Sydney school.* Inaugural lecture at Sydney University Arts Association.
- Martin, J. R. (2001). *Language, register and genre.* In A. Burns & C. Coffin (Eds.), *Analysing English in a global context: A reader* (Uk. 149-166). Routledge/Macquarie University/ The Open University
- Massamba, D. P. (1986). “On the influence of Local Languages on Kiswahili: The Case of Mara Region in Tanzania.” *Journal of The Institute of Kiswahili Research. UDSM VOL. 53/1&53/2 1986.*
- Mazrui, A. & Mazrui, A. (1993). “Dominant Languages in a Plural Society: English and Kiswahili in Post-colonial East Africa.” *International Political Science Review. Vol. 14, 3 Uk. 275-292.*
- Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Development, Research and Literature.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa.* Nairobi: Educational Research and Publications.
- Mukuthuria, M. (2006). “Kiswahili and its expanding Roles of Development in East Africa: A Case of Uganda.” *Nordic Journal of African Studies 15(2):* Uk. 154-165.
- Morgan D. L. (2008). *The SAGE Encyclopedia of Qualitative Research Methods.* SAGE Publications, Inc. Uk. 816–817.

- Mulokozi, M. (1989). "English versus Kiswahili." In *Journal of Linguistics and Language in Education*. 4 (2): 116-131.
- Mulwale, B. M. (2008). "Kiswahili and Sustainable Environmental Management in Bungoma District, Kenya." In J.B Ogone & D.O. Orwenjo (wh), *Text Language and Literature: Empirical and Theoretical Perspectives from Kenya*. Saasbruken: V.D.M.
- Mutiga, J. (2005). "The Impact of a National Language on other indigenous Languages: The Case of Kenya," *Katika DAAD. A CrossBorders: Benefiting from Cultural Differences* (Uk. 236-249). Nairobi: DAAD Regional Office for Africa.
- Myers-Scotton, C. (1993). *Social Motivations for Code-Switching: Evidence from Africa*. Clarendon Press.
- Nekvapil, J. (2011). The history and theory of language planning. In E. Hinkel (Ed.), *Handbook of research in second language teaching and learning* (Vol. II, pp. 871–887). New York, NY: Routledge.
- Nekvapil, J. (2006). 'From Language Planning to Language Management', *Sociolinguistica*, 20, 92–104
- Ogechi, N. O. (2003). "On Language Rights in Kenya." *Nordic Journal of African Studies* 12(3): 277-295.
- Okombo, D. O. (2001). "Language Policy: The Forgotten Parameter in African Development and Governance Strategies," *Inaugural Lecture*, University of Nairobi.
- Otsuji, E & Pennycook, A. (2010). *Metrolingualism: Fixity, Fluidity and Language in Flux. International Journal of Multilingualism*, Vol. 7, pg. 240 -254
- Paltridge, B. (2001). *Genre and the Language-Learning Classroom*. Michigan: University of Michigan Press.
- Prah, K.K. (2002) *Researching African Languages for Specific and Technological Development: The CASAS Experience*. In F.O Rew (mh), *Speaking African: African Languages for Education and Development* (pg. 9-16). CASAS
- Province, N. W., & Kretzer, M. M. (2018). *Language Attitude for the Use of Indigenous Language at Primary Schools in South Africa: A Case Study in Gauteng and North West Province: The Arts and Indigenous Knowledge Systems in Modernized Africa*, 245.
- Republic of Kenya (2010). *The Constitution of Kenya*. Government Printer.
- Republic of Kenya, (2011). "Developmental Devolved Government for Effective and Sustainable Counties." *Sessional Paper on Devolved Government of Kenya*. Office of The Deputy Prime Minister and Minister for Local Government.
- Ricento, T. (2000). Historical and theoretical perspectives in language policy and planning. *Journal of sociolinguistics*, 4(2), 196-213.
- Romaine, S. (2006). "Reversing Language Shift and the future of linguistic diversity: where ideology and theory meet". *Workshop on Language Ideology and change in Multilingual Communities*. Seminar Paper, University of Carlifornia, San Diego.
- Rowland, A., & Flint, J. (2004). *Encyclopedia of Social Science Research Methods*. SAGE Publications, Inc. Uk. 1044–1045.
- Ruiz, R. (1984). "Orientations in Language Planning." *NAB Journal* 8 (2). Uk. 15-24.
- Salkind, N. J. (2010). *Encyclopedia of Research Designs*. Thousand Oaks, CA: Sage.
- Sebba, B. (2011). Societal Bilingualism. In Wodak, R., Johnstone, B. & Kerswill, P. (Ed)., *The Sage Handbook of Sociolinguistics*. Sage Publications Ltd. <https://dx.doi.org/10.4135/9781446200957>.
- Simiyu, V. G. (1985). "The Emergence of a Sub-nation, Bukusu of Bungoma." Makala ya Seminaa: Bungoma 3rd- 5th Disemba.
- Shitemi, N. L. (2011). *Kubidhaaisha na Kuwezesha Lugha Kama Sarafu ya Kiuchumi: Kielelezo cha*

- Taaluma ya Kiswahili na Tafsiri. Eldoret: Moi University Press.
- Shohamy, E. (2006). *Language Policy: Hidden Agendas and New Approaches*, Abingdon, Routledge.
- Skutnabb-Kangas, T & Harmon, D. (2018). Biological diversity and language diversity: parallels and differences. In Penz, Hermine & Fill, Alwin (eds). *Handbook of Ecolinguistics*. New York: Routledge, 11-25.
- Spolsky, B. (2009). *Language Management*, Cambridge, Cambridge University Press
- Spolsky, B. (2007). "Towards a Theory of Language Policy." *Working Papers in Educational Linguistics*, 22/1: Uk. 1-14.
- Spolsky, B. (2004). *Language Policy*. Cambridge: Cambridge University Press
- Sure, K. (2002). "Language Planning and National Development in Kenya," In I. Risson (Ed): *Language Contract* (Uk. 23-37). Bayreuth: Eckhard Breitingger.
- Tosco, M. (1992). Dahalo: An endangered language in M. Brenzinger (mh) *Language Death: Factual and Theoretical explorations with special reference to East Africa*. Berlin: Monton de Gruyter.
- UNESCO, (2003). *Education in a Multilingual World*. Paris: United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.
- UNESCO, (1996). *Universal Declaration of Linguistic Rights*. Barcelona: United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.
- Wardhaugh, R. (1987). *Languages in Competition: Dominance, Diversity, and Decline*, Oxford, Blackwell
- Wardhaugh, R. (1987). *Languages in competition: Dominance, diversity, and decline*. Wiley-Blackwell.
- Webb, V. (2002): *Language in South Africa: The Role of languages in National Transformations reconstruction and development*. Pretoria: John Benjamins Publishing Company.
- Webb, V. & Sure, K. (2000). "Language as a Problem in Africa," Katika V. Webb & K. Sure. *African Voices: An Introduction to Linguistics of Africa*. Oxford: Oxford University Press.
- Wolff, D. (2000). Second Language Writing: a Few Remarks on Psycholinguistic and Instructional Issues. *Learning and Instruction*, 10, 107-112.
- Yeh, H., Chan, H. & Cheng, Y. (2004). "Language use in Taiwan: Language Proficiency and Domain Analysis," *Journal of Taiwan Normal University: Humanities and Social Sciences* 49 (1) Uk. 75-108.